

KUJIVUA UANACHAMA WA CHADEMA

1. Kazi kubwa ya chama chochote cha siasa ni kujiandaa na hatimaye kushinda uchaguzi ili kiweze kuunda na kuendesha serikali/dola kama njia ya kutekeleza maono yaliyo kwenye ilani yake ya uchaguzi kwa lengo la kuleta maendeleo na ustawi katika nchi. Chama hufikia lengo hili kwa kutoa *falsafa, sera* na *uongozi makini* na bora zaidi kuliko vyama vingine ili wananchi wakiamini na kukichagua.
2. Nilijivua uanachama wa CCM mwaka 2015 na kujiunga na CHADEMA nikiamini kuwa nitashiriki kukifanya chama hiki (CHADEMA) kikomae na kufikia hatua ya kuwa chama mbadala kifalsafa, kisera na kiuongozi. Hata hivyo, uzoefu wangu wa miaka miwili tangu nijiunge na CHADEMA umenionesha kuwa kama chama bado kina safari ndefu kisiasa kuwa chama mbadala kwa lengo la kuunda serikali imara na inayowajibika kwa wananchi. Mpaka sasa chama kimeendelea kujikita katika kukosoa na kuonyesha madhaifu ya serikali, na hasa Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli binafsi. Natambua kwamba kukosoa ni kazi muhimu ya chama cha upinzani, kazi hii pekee haikifanyi chama kuwa chama mbadala cha kuunda serikali.
3. Aidha, si sahihi kwa vyama vya upinzani kuwekeza katika kumpinga Mh. Rais John Pombe Magufuli, ambaye ni Rais pekee anayetekeleza kwa vitendo mambo mengi ambayo upinzani wameyapigia kelele kwa miaka mingi, ikiwemo tatizo kubwa la ufisadi na uzembe katika utumishi wa umma. Haya ni mambo ambayo hata viongozi waliotangulia ndani ya chama chake cha CCM walishindwa kuyatekeleza kwa ufanisi.
4. Kutokana maelezo ya hapo juu, nimejiridhisha pasipo shaka kuwa upinzani wa sasa nchini Tanzania hauna nia wala sababu ya kutafuta fursa ya kuunda serikali kupitia falsafa, sera na uongozi mbadala. Nimejiridhisha kuwa upinzani wa sasa umeridhika na hali ya kuendelea kuwa wakosoaji ili kuisaidia CCM kujirekebisha. Upinzani hauwezi kutegemea kushika dola kwa kutegemea madhaifu ya CCM badala ya uwezo wake kama mbadala.
5. Kwa hiyo basi, Mimi Lawrence Kego Masha, kuanzia tarehe ya tamko hili, ninajivua uanachama wa CHADEMA. Ni imani yangu kwamba uamuzi huu utanipa fursa ya kutafakari kwa kina safari yangu kisiasa ndani ya nchi hii. Nawashukuru viongozi wa CHADEMA kwa miaka miwili ya kufanya kazi pamoja na nawatakia kila la

Khern

Lawrence Kego Masha

Jumanne 14 Novemba 2017.

Head Office:
Plot No: 1736, Kahama Road, Masaki,
P.O. Box 106204, Dar es Salaam, Tanzania
T: +255 22 260 1268 | M: +255 684 904 444
F: +255 22 260 1269 | info@gabrielco.legal

Arusha Branch Office:
Plot No: 39, LDA, Engira Road, Themu,
P.O. Box 10620, Arusha, Tanzania
+255 732 975 371 | info@gabrielco.legal